


MUNGU HUTAMBULIWA

KWA TABIA ZAKE

 Baba wa Mbinguni, twakushukuru kwa uweza wa kutuongoza hapa Beaumont, Texas, tena. Ninapotazama hapa na pale katika hizi roshani, nakumbushwa nyakati tulipokuwa hapa hapo awali, na maajabu uliyoyafanya, bila shaka wengi wa hao watu wanaketi hapa usiku huu. Kama hungaligusa miili yao migonjwa, hawangelikuwa hapa usiku huu, lakini uliwagusa, nao wako hapa. Ukumbusho mwingi unadumu, tutaenda nao wote Utukufuni.

² Twaomba utupe kumwagwa kukuu kwa Roho. Tubariki sote pamoja. Bariki kila kanisa, kila mshiriki.

³ Na, Bwana, hasa mbariki ndugu wetu mchanga na mpendwa aliye hapa, Ndugu Pearry Green, atanguliaye mbele akijaribu kueleza Hili. Na watu wa—wa mji huu mzuri waone vile huyu kijana anavyo—anavyojisikia kuhusu watu wa hapa, awalete kwa Kristo ampendaye. Naye anajaribu kuingiza kila huduma anayodhani kuwa ni ya kweli, ambayo amechunguza kwa Neno, naye ataka kuona watu wameokolewa.

⁴ Tusaidie Baba, katika juhudi zetu, tunapojitolea Kwako kwa utumishi, kwa heshima na utukufu wa Mungu. Twaomba katika jina la Yesu. Amina.

⁵ Sasa, na ukumbuke kila usiku sasa, mlete mtu fulani, au piga simu na kumwarifu mtu fulani, na umwambie kila mchungaji, kila kanisa. Haijalishi ni lipi, hata kama wanatofautiana nasi, mradi tu mwingie, mketi, mwe na adabu na mwe wema, hakika twafurahia kuwako kwenu hapa.

⁶ Na sasa mlete Biblia zenu, leta kalamu, ketini, mkaandike somo. Enda litafute, lichunguze kwa Neno na uone kama liko sahihi au la. Waona? Na ndipo usichukue theologia yako mwenyewe, lichukue tu vile Biblia imeandikwa. Mwaona, mara nyingi twaweza kusema, “Lamaanisha *hiki*, hiki ndicho linachomaanisha.” Mungu hahitaji mfasiri ye yote, Yeye hufasiri Neno Lake Mwenyewe, Mwaona?

⁷ Mungu alisema, “Iwe nuru,” ikawa nuru. Hilo halikuhitaji—halikuhitaji tafsiri yo yote. Yeye...Lilitendeka jinsi Yeye alivyosema. Yeye alisema, “Bikira atachukua mimba,” naye akachukua. Hilo halihitaji tafsiri yo yote.

⁸ Mungu ameahidi vitu fulani kwa wakati huu ambavyo ni lazima vitimie! Yeye alilisema, halikuhitaji tafsiri basi. Mungu alisema hivyo, naye hutafsiri, Mwenyewe, kwa hivyo basi Biblia

ilisema si ya kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Mungu hufasiri Neno Lake Mwenyewe kwa kulithibitisha.

⁹ Sasa nashangaa ikiwa twaweza kusimama tunaposoma Neno Lake, kutoka katika Kitabu cha Waebrania, sura ya kwanza. Sababu ya kuwauliza msimame ni kwa heshima ya Naeno hili. Naaamini kuwa Neno ni Mungu, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwa kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” “Yesu Kristo Yeye Yule jana, leo, na hata milele,” hicho ndicho kiini cha mikutano yetu. Kwa hivyo, tunapomsoma Mwenyewe aliyepigwa chapa hapa katika Neno hili, twasimama. Tunaponyesha utiifu kwa bendera, bendera yetu inapopita, sisi husimama kuiheshimu bendera yetu, taifa letu, lazima tufanye hivyo. Naam, basi, si yatupasa kusimama hata zaidi tunaposoma Neno la Mungu! Waebrania 1:1-3, tunaposoma.

Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,

Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.

Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akavichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa ukuu huko juu;

¹⁰ Na tuombe. Wangapi sasa, vichwa vikiwa vimeinamishwa pamoja na mioyo, wangependa kukumbukwa katika maombi, ili kupitia kwa huu mkutano, mahali fulani, Mungu atatekeleza matakwa yenu? Hebu inueni mikono yenu. Bwana aiona mikono yenu.

¹¹ Baba yetu uliye Mbinguni, kulingana na kuona kwa macho yangu ya kibinadamu, kulikuwa na mikono mingi. Hakika ufunuo wa Ndugu Green na shauku yangu ya kuja, zilikuwa za kweli. Sasa, Baba, uwape mahitaji yao, kulingana na Neno Lako na Ahadi Yako. Twawakabidhi Kwako. Nayoy maisha yetu yalingane na Neno sana, hata Neno litafanyika mwili kati yetu na liwape watu imani wapate kutoa kwa akiba yao Mbinguni, ambayo Yesu aliwalipia zamani, kwa ajili ya dhambi na magonjwa yao, kwa vile wako safarini. Tubariki sasa, twaomba, tunapokungojea Wewe utufunulie sisi Neno Lako, na kulifanya mwili kati yetu. Kwa maana twaomba katika Jina la Yesu. Amina. (Ketini)

¹² Sasa ningependa, ikiwa mngejaribu, msizungukezunguke hapa na pale zaidi ya vile inawalazimu, namaanisha kusimama na kuondoka, hadi baada ya dakika arobaini na tano au hamsini hivi.

¹³ Sasa, ile—ile juhudi, jambo ni hili, twataka kujua Ukweli ni nini. Na huo ndio Ukweli Mmoja pekee niujuao, nao ni Biblia.

Sasa, Mungu atahukumu ulimwengu siku moja, twaamini hilo, na kila mmoja wetu sisi binadamu ataletwa katika Uwepo Wake ili ahukumiwe. Nina maandishi machache nimeyaandika hapa, na Maandiko ninayotaka kutaja katika dakika chache zijazo.

¹⁴ Sasa kumbukeni, kama ningeuliza usiku huu, “Kuna “Mkatoliki hapa?”

“Naam,” wangesema. Na pengine . . .

“Vema, Mungu atatumia nini kuuhukumu ulimwengu?”

Wangesema, “Kanisa Katoliki.”

¹⁵ Ningemwuliza, “Kanisa Katoliki gani?” Hawasikizani. Kuna kutosikizana kwingi. Moja la Kirumi na lingine la Kiyunani, na la Orthodox, na kadhalika. Tunayo mengi. Kama ningesema . . .

¹⁶ Mmethodisti wangesimama, wakisema, “Atahukumu kulingana na kanisa la Kimethodisti. Vema, ikiwa ni hivyo, basi Mbatisti hana nafasi. Na wakihukumu kulingana na la Kibatisti, basi Mmethodisti hatakuwa na nafasi.

¹⁷ Kwa sababu, kumbuka, kugeuza kwa Neno kidogo tu, moja (siyo lote, si kifungu chote), ni kipande kimoja kidogo tu cha kutokuamini Neno, kulisababisha kila kifo, kila ugonjwa, kila huzuni. Huyo alikuwa Hawa katika Bustani ya Edeni. Sasa ikiwa . . . Hayo yote yaligharimu hayo, kwa mwanamke mmoja tu kuelewa Neno kwa kosa. Yeye hakukusudia kukosea, “alidanganywa,” Biblia ilisema. “Kudanganywa,” kwa Neno, kulisababisha haya yote, basi mimi na wewe hatutarudi na cho chote ila Neno lote.

¹⁸ Sasa, naamini, Biblia yasema kuwa Yeye hawezi, siamini kuwa Mungu atahukumu ulimwengu kulingana na kanisa la Kipentekoste, wala la Kimethodisti, Kibatisti, wala Kikatoliki. Atauhukumu kwa Yesu Kristo, Yeye alisema hivyo. Na Kristo ni Neno, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, hata milele.”

¹⁹ Haya yote ni Milele kuu. Milele haikuanza na wala haiwezi kuisha. Kwa hivyo, katika Huyu mkuu wa Milele kulikuwa na sifa, kuwa Baba, kuwa Mwana, kuwa Mwokozi, kuwa Mponyaji na vitu hivi vyote vilikuwa ndani Yake. Na kitu pekee kinachotendeka sasa, kinaonyesha sifa Zake. Hayo tu.

²⁰ Sasa, majina yetu yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana Kondoo kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na Neno linapogusa hiyo, kama kuna nuru yo yote humo iliyokusudiwa Uzima, Yesu alisema, “Hakuna mtu ajaye kwangu asipovutwa na Baba yangu, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Kwa hivyo waona, ni Neno, kila mara, Neno, Neno.

²¹ Sasa, nataka kunena usiku huu kuhusu somo, nikitoa somo kutoka kwa vifungu hivi ambavyo tumesoma, *Mungu Hutambuliwa Kwa Tabia Zake*.

22 Sasa, karibu kila kitu tunachopata chaweza kutambuliwa kwa tabia zake.

23 Sasa, twona, kama maisha ya wanyama, chukua kwa mfano maisha ya ndege. Sasa, chukua kama kore anapopuruka, na ndege aliye kama kunguru mdogo, wanafanana sana. Lakini tabia za kore, yeye hupunga mbawa zake na kushuka, na tena juu chini juu chini. Hiyo ndiyo tabia yake. Ukichunguza, ndege huyo aliye kama kunguru mdogo huruka moja kwa moja hata aendako.

24 Tazama tomboroko anaporuka, kwale mdogo, arukavyo. Mtazameni kwale wa aina ya Gambe, arukapo, enyi wawindaji. Mwaona, kuna tofauti. Tazama sululu na kitwitwi, zile tabia huamua jinsi alivyo.

25 Kondoo mkuu akisimama mlimani, akiwa ametazama mbele, sehemu ya nyuma ya tako lake ni nyeupe, sehemu hiyo nyingine ni ya kijivu. Kama haukujua tabia za huyo kondoo, huenda angekuwa kulungu. Waona? Waona, lazima ujue tabia zao, kugundua—yupi aliye na yupi asiye. Ni mambo mengi ambayo tungeendelea kuwaeleza kuhusu maisha ya wanyama.

26 Ndipo tunafikia maisha ya wanadamu, tabia kati ya mwanamume na mwanamke. Kuna tofauti. Wote ni wanadamu, bali tabia zao kuwa wa kiume au wa kike huwatambulisha. Wakati mwingine nilikuwa nikisoma baadhi ya mafumbo yaliyowekwa kwa—kwa kumjaribu Suleimani, na yule malkia, ya kuwa alikuwa na wanawake waliovalia kama wanaume. Naye Suleimani akawafanya watembe na kutenda mambo machache, mara akasema, “Hawa ni wanawake.” Waona, kwa sababu angewatambua kwa jinsi walivyotenda, kwa kuwa zile—zile tabia zao zilikuwa za wanawake. Kuna kitu fulani kulihusu ambacho huwezi kukificha, ni—ni mwanamke kwa sababu tabia zake—zake zamtambulisha kuwa mwanamke.

27 Ni kama mkono wa kuume na wa kushoto wa watu. Wote ni watu. Tazama, mmoja hutumia mkono wa kuume na mwingine mkono wa kushoto. Tazama jinsi tabia zao zinavyowatambulisha, waweza kutambua kama wao hutumia mkono wa kuume ama wa kushoto au la. Waona? Bali wote wana mikono, yote miwili yafanana sana, yafanana sana.

28 Naweza kutaja kitu fulani hapa. Yesu alisema, katika Mathayo sura ya 24, kuwa “Katika siku za mwisho, hizo roho mbili zingefanana sana hata zipate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.”

29 Sasa hivyo ni kama kutazama mkono wa kulia na wa kushoto. Yote ina vidole gumba, vidole, makucha, vidole vidogo, vidole vya kati, na vinginevyo, vidole vya shahada, vyote ni vidole tofauti. Hivyo, vyote vina alama sawa, ila vingine vinaelekea upande mmoja na vingine mwingine, vyote vina alama sawa, viliundwa kwa njia ile ile, alama za vidole. Kila

kitu kinafanana, kabisa, tofauti pekee ni tabia yake. Moja ni mkono wa kushoto na mwingine ni mkono wa kuume, hiyo ndiyo tofauti pekee.

³⁰ Na hivyo ndivyo vile roho zitakavyokuwa katika siku za mwisho, zitakuwa, ni tabia yake tu itakayoonyesha kama ni ya Mungu au la. Moja itakuwa ya Kweli na nyingine itakuwa ya uongo, utaitambua tu kwa tabia za Mungu. Kwa ukamilifu, lazima itakuwa hivyo. Lakini mkono wa kuume, tungesema ni wa “Kweli,” na wa kushoto ulikuwa wa “uongo”, waona, au, vinginevyo, mojawapo. Zatambuliwa kwa tabia zao. Waweza kujua tu kwa tabia yao.

³¹ Ni kama tu walivyokuwa Israeli katika safari yao, wakitoka Misri. Naam, Mungu alikuwa pamoja na Israeli, alikuwa amewaonyesha ishara kuu huko, alimtuma nabii kwao na kuthibitisha Neno Lake lililoandikwa. Naye alipowaondoa, twaona tabia Zake, jinsi alivyokutana na Musa, vitu ambavyo alifanya. Na kule, njiani, walifikia taifa lingine, lililokuwa Moabu. Na Moabu lilikuwa taifa kuu, naam, si la kikafiri, kwa vyo vyote vile. Walikuwa watoto wa binti za Lutu, nao walikuwa waamini. Sasa, chunguza mataifa haya mawili. Moja wapo ni taifa linalojulikana na lingine ni la wasafiri tu. Na sasa wakaja mahali ambapo hili taifa kuu la Moabu lilikuwa katika njia yao ambayo wangalipitia, wakienda kwenye nchi ya ahadi. Naam, walikuwa na . . .

³² Tazama yale—yale mataifa mawili, kila moja lilikuwa na nabii. Mmoja wao alikuwa mwalimu mkuu na nabii, Balaamu. Yule mwingine alikuwa Musa. Basi Balaamu yuashuka kutoka . . . kuwalaani Israeli.

³³ Na tazama, wote wawili walikuwa wa kiasili halisi. Ule unabii, wa asili toka kwa Balaamu, ulisema, “Nijengee madhabahu saba,” hiyo hakika ni nambari ya Mungu. “Na juu ya kila madhabahu toa dhabihu safi ya fahali,” ambayo ni dhabihu ile ile walioitoa katika kambi ya Israeli. Naye alisema, “Juu ya kila madhabahu toeni kondoo dume pia,” akinena kuhusu kuja kwa Kristo. Na huko kwa Israeli walitoa dhabihu ile ile.

³⁴ Madhabahu yale yale, Mungu yule yule, ila mojawapo ilikuwa isiyo ya kweli na ile nyingine ya kweli. Na sasa njia ya pekee ambayo ungetofautisha ni ipi ilikuwa. . . Ilipofikia, kiasili, kwa Neno, wote wawili walikuwa sawa. Lakini, mwaona, mmoja, kusudi lake lilikuwa baya, yeye alikuwa akijaribu kumwondosha nduguye kwa ahadi ile Mungu aliyompa.

³⁵ Jambo lingine, mmoja, nabii wa Baalamu, alikuwa wa kiasili, bali yule nabii Musa alitambulikana kwa tabia za Mungu. Kulikuwako ile Nguzo ya Moto, Nuru ya Kimbinguni ikining’inia juu yao. Na kulikuwa na uponyaji mkuu kambini mwao, Mungu wa Kimbinguni akionyesha ishara za kimbinguni. Nao walikuwa wakidumu hasa na lile Neno la ahadi ambalo

Mungu alimpa Ibrahimu kule nyuma wakati mataifa hayo mawili yalipoanza. Lakini, sasa, Musa alikuwa na ahadi ya Ibrahimu, kuenda katika nchi ya ahadi. Balaamu, aliyekuwa pia nabii wa Mungu, akisimama huko. Na njia pekee ambayo ungewatambua, si kutokana na mafundisho yao ya kiasili, bali ni kwa tabia za Mungu.

³⁶ Kulikuwa na mlilo mkuu wa—wa sauti ya Mfalme hapa akiwa pamoja na Israeli. Upatanisho ulikuwa ukitenda kazi, Nyoka wa Shaba, Mwamba uliopigwa. Na Mungu akiwa pamoja nao, akijitambulisha Mwenyewe katika Nuru ya Kimbinguni, na kuponya magonjwa yao na maradhi yao walipokuwa safarini. Tabia zilizithibitisha jinsi Yeye alivyokuwa, wakidumu katika Neno la wakati huo, la wakati walimokuwa wakiishi. Tabia za Mungu zikijidhihirisha Zenyewe katika Musa. Mwaona, tabia za Mungu zilijidhihirisha katika Musa. Nguzo ya Moto, upatanisho ukitenda kazi, maajabu, Mwamba uliopigwa, nao... pia ile Nyoka ya Shaba, ikinena kuhusu uponyaji, na tena—tena pia walikuwa wakitimiza wajibu wao, wa ahadi ya Mungu.

³⁷ Tena, tabia za Mungu si za kawaida. Tabia za Mungu ni za kimbinguni, kwa sababu Yeye ni Muumba. Yeye ni wa Kimbinguni. Na tabia za Mungu ziazapo kujionyesha Zenyewe, ni jambo lisilo la kawaida kabisa kwa mawazo ya kisasa hata huzitupilia mbali. Wao hawawezi kuelewa, bali Yeye haziachi ahadi Zake. Mungu katika wakati wote, nimesema, aligawanya Neno.

³⁸ Hebu na tumchukue, kwa mfano, mmoja. Kulikuwepo Yusufu, mumewe Mariamu. Na sasa yeye alikuwa amemposa huyu msichana, na ilikuwa waoane. Lakini kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

³⁹ Sasa, sote twaamini hayo, ikiwa tu Wakristo. Lazima tuamini hilo ili tuwe Wakristo. Hiyo ni Biblia. Lazima uamini kila Neno katika Biblia, ili uwe Mkristo. Sasa, kwa sababu ikiwa Roho Mtakatifu yuko hapa, ataitikia kila Neno na kila ahadi kwa “amina”.

⁴⁰ Kwa sababu, sasa, Yusufu alikuwa mtu mwenye haki, yeye alikuwa mtu mzuri. Na bila shaka Mariamu alikuwa amemwambia kuhusu kujiwa na Gabrieli, na jinsi Roho Mtakatifu angemfunika kama kivuli, na angepata mimba na kumzaa Mwana, na jina lake angeitwa “Yesu”, bila shaka alimwambia Yusufu hayo. Na Yusufu angetazama katika macho yake makubwa ya rangi ya hudhurungi, naye angeona hayana hila, alitaka kuamini hilo. Yeye alitaka kuliadini kwa moyo wake wote, bali lilikuwa lisilo la kawaida kabisa, naye aliazimu kumwacha, kwa siri.

⁴¹ Sasa, kama mtu ni mnyofu katika hilo, Mungu atafanya njia fulani kumwonyesha mtu huyo kuwa ni Kweli. Yeye ana

wajibu huo, ukiwa u mnyofu. Bali ukiiona, na kuiondokea, basi utahukumiwa. Lakini, ikiwa u mnyofu na unaona Ukweli!

Sasa, Yusufu “aliazimia” tu. Yeye alisema, “Si la kawaida kabisa!”

⁴² Hivyo ndivyo ilivyo leo, kuwa watu, watu wazuri, wapole, waungwana, wahudumu wazuri, wengi wao, makasisi na wengineo, ni watu wazuri, lakini thibitisho la Kimbinguni la ahadi ya siku hizi ni lisilo la kawaida kabisa, huwakwaza sana. Linafanya hivyo kwa sababu linaonyesha tabia ya Mungu.

⁴³ Basi, Yusufu, mumewe, akiwa mtu mwenye haki, hakutaka kumwaibisha. Yeye hangeliimini; yeye—yeye alijaribu kuliimini. Basi alipokuwa akifikiria hayo, Malaika wa Bwana akanena naye na kumwambia.

⁴⁴ Naam, Yeye si lazima anene kila mara katika ndoto, Yeye aweza kujifunua Mwenyewe kwako kwa Neno, na akuonyeshe wewe kuwa ni kweli, ikiwa u mnyofu kutosha kulichunguza na kuona ikiwa ni tabia ya Mungu inayojonyesha Yenyewe, lakini kila mara kulingana na Neno lililoahidiwa.

⁴⁵ Na jambo lingine, Neno la Mungu kila mara husahihisha kosa. Mwaamini hilo? Neno latosheleza. Mungu anapothibitisha Neno hilo, hilo latosheleza.

⁴⁶ Sasa hebu, ningalitaka kuwaza mmoja tu mawazoni mwangu. Hatutachukua muda mwingi sana, kwa sababu twataka kuwaombea wagonjwa. Tuone wakati. . . Yesu akiwa Neno, Biblia ilisema Yeye alikuwa Neno. Sote twakubaliana na hilo, kuwa Yeye alikuwa Neno. Tazama Yeye alipokuwa na Umri wa miaka kumi na miwili. Sasa, hatuna habari kwamba alienda shuleni. Lakini mtoto wa kiume wa miaka kumi na miwili wa urefu kama huu, wao, wazazi Wake, Mariamu na Yusufu walienda hekaluni ku. . . huko—kuabudu siku ya Pasaka. Nao walipokuwa huko, walisafiri kurudi nyumbani baada ya pasaka, walisafiri kwa siku tatu, nao wasimpate Yesu po pote. Na mwishowe walimpata baada ya kumtafuta kwa siku tatu, hekaluni, akibishana na wazee kuhusu Neno la Mungu.

⁴⁷ Basi msikieni Mariamu sasa. Naam, kwa watu wanaomchukua kuwa mungu wa kike, tazameni. Mwaona, mwanamke ndiye aliyedanganywa mwanzoni. Na mtazameni hapa. Kama hujalion, tazama hili. Yeye alisema, “Baba yako nami tumekutafuta kwa machozi.” Tazama, yeye alilaumu ushuhuda (mbele ya makuhani hao) aliushuhudia. Alisema kuwa “alipata mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu,” na hapa yeye alimwita “Yusufu” baba Yake.

⁴⁸ Sasa mtazame huyo mvulana wa umri wa miaka kumi na miwili, akiwa Neno la wakati huo. Yeye alikuwa Neno lililoahidiwa kwa wakati huo, Masihi mpakwa mafuta. Tazama yale Yeye aliyosema, “Hamjui kwamba yanipasa nitende kazi ya Baba Yangu?” Neno lasahihisha kosa. Mwaona, na ni

ya Kimbinguni, mtoto wa umri wa miaka kumi na miwili! Sidhani kuwa Yesu alifahamu yale aliyoyasema, lakini Yeye alikuwa Neno, na Neno husahihisha kosa. Mwaona, Yeye alimsahihisha mamake, na kumkemea kwa kusema hivyo. Sasa, kama ingekuwa—ingekuwa kazi ya babake, Yeye angekuwa pamoja na baba Yake, ikiwa Yusufu alikuwa baba Yake.

⁴⁹ Lakini, mwaona, yeye akiwa amevunjika moyo na kuhangaika, kama Hawa alivyokuwa, na kushawishika, naam, yeye alisema, “Baba yako nami tumekutafuta, kwa machozi.”

⁵⁰ Yeye alisema, “Hamjui kuwa lazima nitende kazi ya Baba Yangu?” Mwaona jinsi Neno ni la kusahihisha, husahihisha kosa.

⁵¹ Shetani alifanya kosa alipojaribu kumjaribu Yesu. Lakini Yeye alimjibu kwa Neno Lake Mwenyewe, na kumshinda kwa Neno.

⁵² “Mungu”, Biblia ilisema hapa, “kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, alijitambulisha Mwenyewe kwa manabii Wake, alisema na baba zetu kwa manabii.” Sasa, akionyesha tabia Zake za kujitambulisha Mwenyewe, mwaona, kwa mwanadamu, Yeye alinena na manabii. Manabiii, maono yao, yaliyothibitishwa, yalikuwa—yalikuwa tabia za Mungu zilizofanywa zijulikane kwa ono la nabii.

⁵³ Sasa, hukuna mtu awezaye kueleza ono, haiwezekani kamwe. Ni jambo la kimbinguni. Ni jambo unaloona jinsi liliyokuwa, lilivyo, na litakavyokuwa. Na hiyo ndiyo iliyokuwa njia ya Mungu, ya kumtuma mtu aliyenena maneno hayo na kuonyesha vitu vitakavyotendeka (si usiku huu tu) kila usiku, kila wakati. Kila kitu yeye alichosema kilipaswa kiwe kikamilifu kwa Bwana, kiwe Neno la Bwana.

⁵⁴ Kwa hili, karama na mwito havina majuto. Hauwezi kuyageuza macho yako yawe ya hudhurungi ikiwa ni ya samawati. Hauwezi kujifanya uwe wa futi sita ikiwa u futi nne. “Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Sisi tuko, wote, vile tulivyo kwa neema ya Mungu.

⁵⁵ Sasa, karama na mwito bila majuto. Hawa manabii walizaliwa manabii. Musa alizaliwa mtoto mzuri. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, kabla misingi ya dunia kuwekwa, sifa ya Mungu. Yereimia . . .-kumi na mbili, miaka mia saba na kumi na miwili, naamini ilikuwa hivyo, kabla Yesu hajazaliwa, Yeye alikuwa sauti ya mtu . . . La, niwieni radhi, Yeye aliwekwa kuwa nabii kwa mataifa, na—alikuwa—na alitakaswa tumboni mwa mama yake na kuchaguliwka nabii kwa taifa. Yohana Mbatizaji, ndiye ninayewazia, ikiwa miaka mia saba na kumi na miwili kabla yeye hajazaliwa. Alikuwa sauti ya mtu aliaye nyikani.

⁵⁶ Mwaona, ni Mungu anayeweka. Yeye humtuma mtu, apeleke Neno la wakati huo. Lakini sasa kabla haujaliamini lile Neno la

wakati huo, Yeye anajitambulisha Mwenyewe katika tabia Zake, Mwaona, kwa maarifa, kwa ono. Yeye alisema vitu ambavyo vingetendeka na vikatendeka. Na Mungu alisema, “Hayo yanapotendeka, basi aminini yeye anatafsiri ya Neno, kwa—sababu Neno la Bwana hufa kwa mtu huyu.” Na stakabadhi zake, yeye anatambuliwa kwa kuwa nabii, katika Agano la Kale. Ni dhahiri tu kama liwezavyo kuwa! Tabia zake hutambulika, zinajulikana, tabia zake.

⁵⁷ Sasa, hivi ndivyo “Mungu alitenda kwa sehemu nyingi.” Biblia yasema, “na katika njia nyingi, alisema na baba zetu katika manabii, lakini katika siku hizi za mwisho kupitia kwa Yesu Kristo, Mwanawe, Yeye husema.”

⁵⁸ Sasa Yesu alisema, katika Yohana 10:37, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini.”

Mwaona, wao walisema, “Wewe uliye Mwanadamu, wajifanya Mwenyewe Mungu.”

⁵⁹ Yeye alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini.” Sasa Yeye alisema, “Yohana alikuwa taa iwakayo na kung’aa. Ninyi, wakuu, mnapenda kuenenda katika nuru Yake kwa kitambo. Sasa Yohana alisema, ‘Sina budi kuondoka, bali Yeye kuzidi.’” Yeye alikuwa Nuru ya ulimwengu, kwa sababu Yeye alikuwa Neno lililodhihirishwa, likatambuliwa na lililofanyika mwili. Mwaona, Yeye alikuwa Mungu pamoja nasi.

⁶⁰ Manabii walikuwa Mungu pamoja nao. Yesu alisema hivyo. Yeye alisema, “Ikiwa mwawaita wale waliojiliwa na Neno la Mungu, “miungu”, mwawezaje kunihukumu ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?” Mwaona? Kwa hivyo mahali ambapo Neno lililonenwa na Mungu linadhihirishwa, basi huyo ni Mungu akijitambulisha Mwenyewe kwa tabia Zake, akitimiza Neno Lake. Halihitaji tafsiri. Limekwisha jitafsiri, Lenyewe, Likathibitisha jinsi lilivyo.

⁶¹ Kama tu vile Yeye alivyosema “iwe nuru” na ikawa nuru, haikulazimu kusema, “Vema, hilo lilimaanisha nini?” Lamaanisha tu hivyo, liko hivyo, hiyo inalithibitisha. Limekwisha kutimia.

⁶² Sasa, Yesu alisema kuwa, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu,” au kwa maneno mengine, “Kama sina tabia za Baba Yangu, msiniamini. Hizo hudhihirisha tabia Zangu, Mimi ni nani. Msiponiamini, basi aminini kitambulisho ambacho Mungu amenipa. Kama nyinyi—kama nyinyi. . . Kama mimi, kama tabia Zangu hazitambulishi Mimi ni nani, basi msiamini madai Yangu.” Mnaona? Mnalipata usiku huu? Wangapi wanalielewa, inueni mikono yenu. Mwaona? “Kama tabia Zangu hazidhihirishi ninayedai kuwa,” Yesu alisema, “basi aminini ile. . . Kama hamwezi kuniamini mimi, basi, aminini kile—kile—kile kitambulisho cha nafsi Yangu.”

63 Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye” Yesu alisema “Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Sasa tazama, “Yeye aniaminiye Mimi,” mwamini wa kweli, “Kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Tazama. Kwa maneno mengine, ni hivi, “Yeye aniaminiye Mimi atatambuliwa kwa tabia Zangu, zile kazi.” Sasa, hayo ndiyo aliyotenda. Yeye alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi.” Na Baba alinena na manabii, na hiyo ndiyo iliyokuwa tabia yao, thibitisho. Vivyo hivyo na Yesu. Na akamuahidia kila aaminiye, Tabia Zangu zitatenda ndani yake kama tu vile zilivyotenda ndani yangu. Nisipotenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Lakini nikizitenda zile kazi, nanyi msiniamini, basi aminini kazi, kwa maana zimenenwa, lazima zitimie.”

64 Yeye alisema, “Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayowaambia mimi ni nani.” Huyo alikuwa Yesu, mnaona, Mungu aliyedhihirishwa, akijionyesha Mwenyewe. “Yanashuhudia Mimi ni nani.” Hilo linafanya Waebrania 1:1 sasa, “Mungu alisema zamani katika manabii,” akionyesha waziwazi sasa zile tabia za kufufuka kwa Mwanawe. Mungu alisema katika manabii zamani hizo, na sasa katika Mwanawe. Mungu asiyebadilika, tabia ile ile,” “Kazi nizifanyazo Mimi, nanyi mtazifanya pia.” Mungu hujulikana kwa tabia Zake zilizodhihirishwa. Hivyo ndiyo umjuavyo.

65 Wasema, “Vema nakwambia hivi, twaimba hivi, twatenda haya, na twatenda.” Sineni hayo.

66 Naongea kuhusu Neno lilidhihirishwa na kuthibitisha Maisha haya, zile tabia za Neno lililoahidiwa kwa wakati huu.

67 Hao Mafarisayo walijua hiyo Biblia vema kama ye yote yule, vema zaidi ya sisi wahubiri tujuayo yetu siku hizi. Wao iliwabidi waitii. Babu zao wa jadi na jadi walikuwa makuhani. Waliisoma kwa makini, mchana na usiku, nao wakakosa kuliona hilo Neno lililothibitishwa.

68 Leo, akasema Luther, “Unapoamini umeipata.” Wamethodisti husema, “Ukiwa na shangwe, umeipata,” Wapentekoste walisema, “Uliponena na lugha, ulikuwa nayo.” Twapata hayo yote si kweli! Wengine wao walisema, “Tunda la Roho linayo.” Hilo ni kosa! Ishara pekee ni, ni wakati inapothibitishwa, Mungu Mwenyewe anapojitambulisha Mwenyewe katika lile Neno la ahadi la wakati. Ndiyo hiyo.

69 Nani aliyekuwa na matunda ya Roho zaidi ya hao makuhani wenye huruma wa kale, waliowatahiri watoto na kuwabariki, na mengineyo? Na hapa huyu mtu Yesu alikuwa, akaja akayapiga teke madhabahu yao, akawatazama kwa hasira, akawapiga, akawafukuza, hakuwa na kitambulisho cho chote. Maandiko ndiyo kitambulisho chake! Hakuwa na kadi ya ushirika, hakuwa

mshiriki wa dhebebu lo lote. Lakini Mungu alinena juu Yake, hicho ndicho kilikuwa kitambulisho Chake!

⁷⁰ Hicho ndicho kitambulisho halisi cha Mungu wakati wo wote, ni kitambulisho Chake. Ndicho hicho, Maandiko yaliyoahidiwa yanapotambulishwa kwa tabia za ahadi ambazo ni Mungu, na Mungu ni Neno. Na zile tabia za hiyo ahadi zinapothibitishwa, hiyo humfanya mwamini. Yesu alisema hivyo, hilo lilitosha. Amina.

⁷¹ Tazama, sasa twatambua, zile tabia zinamtambulisha Yeye. Kama Yeye alivyosema, “Ikiwa hazinitambulishi, basi msiniamini.” Sasa, Yesu alisema kuwa zingemtambulisha.

⁷² Na sasa kumbuka, kuwa katika siku hizi, siku hizi za mwisho, inasema Waebrania 1:1, “Mungu, ambaye kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi alisema na baba zetu katika manabii. Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana Wake Yesu Kristo.” Mwaona? Kutambulikana kwa Mungu Mwenyewe akidhihirishwa katika njia ile ile kama alivyofanya zamani, akitumia tabia zile zile Zake. Amina. Tazama Waebrania 13:8, yasema, “Ni yeye yule jana (kwa sehemu nyingi) leo, na hata milele yule yule!” Hali Yake ile ile, njia Zake zile zile, tabia Zake zile zile, kila kitu sawa! Mungu, asiyebadilika hawezi kamwe kuacha tabia hiyo kama Yeye asivyoweza kuacha Amri Zake. Hivyo ndivyo Yeye alivyo, Yeye ni Neno. Yeye—ni Neno la wakati huu. Yeye ni Neno alipoumba nchi, hilo lilikuwa Neno. Alipomumba mwanadamu, hilo likukuwa Neno, sifa Zake. Alipomuumba Kristo, huyo alikuwa Mungu, Imanueli. Naye alipomfanya Mwokozi, hizo zilikuwa sifa Zake. Alipomfanya Mponya, hizo zilikuwa sifa Zake. Mnaona? Ni Neno kila wakati likithibitishwa, Neno lililothibitishwa kwa tabia za Mungu. Tazama hiyo hali, Yeye daima, habadiliki Kamwe.

⁷³ Watazame wale watu watatu waliomjia Ibrahimu, akiketi katika mlango wa hema yake siku hiyo. Tutamtazama pale kwa dakika chache. Yeye alikuwa amekuja, alikuwa ameitwa aondoke katika nchi ya Keldayo, Wakaldayo, na mji wa Uru. Yeye alikuwa ameondolewa katika mji wake, kwa Maagizo ya Mungu, kwamba ajitenge mwenyewe na kila kutokuamini. Hiyo ndiyo tabia ya kwanza ya Mungu, ujitenge na kutokuamini, amwitapo mtu!

⁷⁴ Naye alimpa kitu fulani, kisichowezekana kabisa, kwa mawazo ya kawaida, kuaminika. Yeye alisema, “Ibrahimu, . . .” Yeye alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, na Sara alikuwa wa miaka sitini na mitano. Wao, huyo likuwa binamu wake, walikuwa wameishi kwa miaka hii yote bila watoto. Yeye alisema, “Nitakupa mtoto kwa Sara, naye atakuwa, katika yeye, nitakufanya baba wa mataifa mengi.” Sasa, yeye aliamini.

⁷⁵ Wakati ukapita, hakukuwa na mabadiliko katika Sara. Mnaona? yeye alikuwa amepita umri, yeye—yeye alikuwa

amekoma kupata hedhi. Miaka sitini na mitano, yeye alikuwa amekwisha pita wakati huo. Ibrahimu, miaka sabini na mitano, mwili ulikuwa kama mfu. Tumbo lake Sara la uzazi lilikuwa kama lililokufa. Lakini Ibrahimu hakusita kamwe katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini. Yeye aliendelea kuamini, kwa sababu Mungu alisema, naye alishawishika, “Kama Mungu alisema, tabia Zake zitatoa kile Yeye alichosema!” Sasa, yatupasa tuwe wana wa Ibrahimu, Mzao wa Ibrahimu! Ikaendelea, ikaendelea, miaka ishirini na mitano ikapita. Hakuna mabadiliko katika Sara, yawayo yote, ila tu alikuwa anazidi kuzeeka, akawa kikongwe, na Ibrahimu pia. Hata hivyo Ibrahimu alizidi kuamini.

⁷⁶ Na siku moja, Mungu alipoona kuwa mtumishi wake alikusudia kuwa kielelezo kwa watu wa siku hizi, na kupitia kwake yeye angewabariki mataifa, asubuhi moja yenye joto yapata saa tano, watu watatu walikuja mpaka kwake. Walimzungumzia. Naye aliwakaribisha waketi. Kulikuwa na kitu fulani kuwahusu kilichoonekana tofauti na binadamu. Vitu vya kiroho hueleweka kwa vitu vya kiroho. Tazama, nao wakaja na kuketi. Ibrahimu akawatazama, yeye akasema, “Bwana Wangu.” Yampasa kufanya nini?

⁷⁷ Wawili kati yao wakashuka kwenda kuhubiri huko Sodoma, ambao ni ushuhuda wa kisasa siku hizi. Tabaka zenu tatu za watu ndizo hizo: Sodoma, na kanisa huko Sodoma, Ibrahimu Mteule hayuko huko Sodoma. Wajumbe wawili, Billy Graham wa kisasa na... Kumbuka, kati ya wajumbe wote wa kanisa, hajawahi kamwe kwenda mtu huko katika makanisa ya kawaida, ambaye jina lake laishia na h-a-m, hapo awali. Kumekuwepo Finney, Sanky, Knox, Calvin, na kadhalika, Billy Sunday, na wengineo, lakini hapana G-r-a-h-a-m, wala ye yote anayeishia h-a-m, ambayo maana yake ni “baba wa mataifa.” Hapo akashuka mle, akihubiri. Utazame wakati huu! Hapo kuna wale wanaojifanya waamini, wasioamini, na waamini. Hawa watu watatu wakaja. Wawili kati yao walienda mjini, Billy Graham wa kisasa na Oral Roberts huko kati ya watu, wakihubiri. Hali hii ya mambo, Yesu aliitaja.

⁷⁸ Tazama, hao Wateule walikuwa wakija, wakiketi nje hapa, Ibrahimu na kundi lake. Na wakati huyu Mtu aliyeketi pamoja na Ibrahimu, mtazame, Yeye alionyesha zile tabia za Mungu kwa kuwa Yeye alisema, “Sara yuko wapi?” Jina lake lilikuwa, Sarai, siku iliyotangulia; sasa ni Sara, S-a-r-a. Kasema Ibrahimu, si Abramu, “Ibrahimu, yu wapi Sara mkeo?”

Akasema, “Yeye yumo hemani nyuma Yako.”

⁷⁹ Akasema, “Nitakuzuru”. Basi Ibrahimu akasikiza maneno hayo. “Nitakuzuru kulingana na wakati wa maisha.”

⁸⁰ Naye Sara akacheka, kama tusemavyo, akacheka kindanindani, moyoni mwake, na kusema, “Niwapo mkongwe,

na bwana wangu mzee, tutapata furaha tena kama vijana wa kiume na wa kike? Kulingana—kulingana na uhusiano wa kibinadamu ulivyo, labda, miaka mingi imepita. Mimi?” Yeye akacheka.

⁸¹ Na Mtu huyo, akimtaazama Ibrahimu, Sara akiwa hemani nyuma Yake, akasema, “Mbona Sara amecheka akisema haya, ‘Haya yawezekanaje?’” Yeye alijitambulisha Mwenyewe.

⁸² Naye Ibrahimu alimwita “Elohim.” Sasa, ye yote kwenu asomaye Biblia ajua hayo. Elohim, Mungu, yule ajitoshelezaye kwa vyote, mnaona, alijitambulisha katika mwili wa mwanadamu uliokuwa ukila nyama ya ndama, ukinywa maziwa ya ng’ombe, na ukila mkate na siagi. Elohim alidhihirisha zile tabia za Mungu, na Ibrahimu alimwita Yeye “Mungu”. Nini? Yeye alithibitishwa, Elohim!.

⁸³ Yesu alisema, katika Luka, sura ya 17, ambapo katika siku za mwisho (Mungu ambaye kwa mara nyingi alisema katika manabii, mwisho wa siku hizi amenena katika Mwanawe), sasa tazama, Yeye alisema, “Wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa.” Tazama, “funuliwa”, kufanywa ajulikane katika hizi siku za mwisho kabla ya wakati wa mwisho, Mwana wa Adamu anapofunuliwa, hali hii ya Sodoma itakuwako tena. Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwa Mwana wa Adamu, wakati anapofunuliwa, akijulishwa kwa Kanisa, kwa walio Wateule (si kwa Sodoma au kwa Wasodoma, wala wale walioko huko Sodoma), kwa walio Wateule.” Ibrahimu alikuwa Mteule. Na Uzao wa kifalme wa Ibrahimu ni walio waamini, katika Kristo Yesu aliye Neno, na ndio walio Wateule. Na wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa, hali hiyo ingekuwepo tena.

⁸⁴ Utazame ulimwengu siku hizi. Kama si Sodoma na Gomora ya kawaida, sijawahi kuona moja. Sodoma na Gomora! Tazama kanisa, kama Lutu akiketi pale na kuhuzunisha tu roho yake takatifu akiona dhambi za Sodoma. Mara nyingi muhudumu akiketi mle, mtu mzuri akiketi katika chumba chake cha kusomea, akitafuta somo lake na mengineyo, anatazama barabarani na kuwaona wanawake wamevalia kaptula, na vitu vya zinaa, na mambo yakiendelea hivyo, hawawezi kusema cho chote kuyahusu, dhehebu lisije likamfukuza. Lutu hakuwa na ujasiri wa kusimamia ya Kweli, ndivyo ilivyo Sodoma na Gomora siku hizi.

⁸⁵ Lakini kuna wengine wa wale walio nje ya Sodoma, waliozaliwa nje huko, si kwa mapenzi ya mwanadamu, bali kwa mapenzi ya Mungu na walio mbegu ya Mungu. Chunguza thibitisho hapo, si kuhubiri tu, lakini ishara ililitambulisha lile Neno la Mungu lililofanyika mwili katika mwanadamu. Ile hali inarudi tu kama vile ilivyokuwa, na ni siku hiyo hasa. Kila kitu ni kikamilifu, kila kitu kiko sawasawa kabisa. Laiti kungekuwa na

wakati wa kuendelea nacho kwa dakika chache, lakini hatuna, kwa hivyo tutaharakisha. Hali hiyo lazima ijiirudie tena katika siku za mwisho.

⁸⁶ Sasa, Waebrania 10:1, “Mungu katika sehemu nyingi alijitambulisha katika manabii. Na katika siku za mwisho amejitambulisha Mwenyewe katika Mwana,” ikimfanya Waebrania 13:8, “yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁸⁷ Tazama Mungu katika sehemu nyingi alinena na Musa. Na sasa, kumbukeni, Yeye alijitambulisha katika Nuru, ile Nguzo ya Moto katika kijiti kilichowaka moto. Hivyo ndivyo alivyofanya katika sehemu nyingi. Naye alinena na Musa. Na hiyo nuru, ilifanyaje? Iitoa tabia za Mungu, ilinena lile Neno, “Nimesikia vilio vya watu Wangu huko Misri. Nimeona kuugua kwao na kusikia vilio vyao, nami nimekumbuka Neno Langu. Nitashuka chini, Nguzo ya Moto, Nuru, niende kuwakombo wa watu hao. Nakutuma wewe, Musa.”

⁸⁸ Chunguza zile tabia za Mungu. Alitwaa vumbi mkononi na kulitupa hewani, na likageuka kuwa viroboto. Tabia za Mungu za uumbaji zilikuwa katika Musa.

⁸⁹ Na Musa alinena, katika Kumbukumbu la Torati 18:15, na kusema, “Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Sasa tazama, hilo ni lile Neno tena, tabia. Mungu akinena katika Musa akiwaambia wao kuwa Bwana angewaondokeshea Mmoja aliye kama yeye. Sasa tazama jinsi tabia za Yesu zilivyomtambulisha Yeye kuwa Neno hilo lililoahidiwa. Wakati Musa alisema ingekuwa, tabia za Yesu zilitambulisha. Tazama, sasa, “Bwana Mungu wenu,” huyo ni Mungu, hilo ni Neno, “atakuondokeshea Nabii kama nilivyo mimi. Ye yote asiyemwamini huyo Nabii, atakatiliwa mbali na watu wake.” Sasa tazama, Yesu alipokuja, basi angekuwa na tabia za aina gani? Mnaona, tazama sasa Neno lililoahidiwa, Yeye aliahidiwa kuwa Nabii kama Musa.

⁹⁰ Sasa, walikuwa na aina zote za waalimu, aina zote za marabi. Hawakuwa na nabii kwa miaka mia nne, tangu—tangu Malaki, na sasa mara tu akatokea mtu.

⁹¹ Sasa, kulikuwepo mvuvi, wawili wao, wana wa mtu fulani, na mmoja wao, jina lake lilikuwa Andrea, na jina la mwingine lilikuwa Simoni. Wao walikuwa wameambiwa na baba yao namna ya kuwa waangalifu sana katika siku hizo; palikuwepo vitu vingi vya uongo vilivyotokea. Yule mzee... Nilikisoma kitabu kidogo siku moja, ambamo, labda kilikuwa cha kubuniwa tu, sijui, ya kwamba, alisema, “Wanangu, sasa kabla tu hajaja Masihi, kama sote tunavyomtazamia, kutakuwepo wakati ambapo kutatukia kila aina ya vitu. Lakini jinsi utakavyomjua huyo Masihi, yeye atakuwa kulingana na Maandiko. Yeye atakuwa Nabii, kwa sababu Neno la Mungu lilisema Yeye yu Nabii.”

⁹² Andrea alimsikia Yohana. Vema, kitu pekee ambacho Yohana alikuwa akifanya, ilikuwa tu ni kutoa unabii. Mwajua, Yesu alisema, “Mlienenda katika nuru ya Yohana, lakini nina Nuru kuu kuliko Yohana. Nina utambulisho mkuu zaidi kuliko Yohana, kwa maana, kazi alizonipa Baba, zanishuhudia Mimi.” Yohana alihubiri tu, yeye alitangulia tu, hakufanya miujiza yo yote au tabia zo zote za Mungu kwa ajili ya ahadi. Lakini hapa yuaja Yesu akiwa na tabia hiyo!

⁹³ Simoni alikwenda kumsikia Yeye siku moja, na mara tu baada ya... Simoni labda alikwenda na Andrea. Andrea alikuwa akihudhuria wakati wote. Lakini, Simoni, alipokuja katika ule Uwepo! Sasa sikia, kwa kufunga. Yeye alipokuja katika Uwepo wa Yesu, Yesu alimtazama, Yeye akasema, “Jina lako ni Simoni, nawe u mwana wa Yona.” Mwaona, ile tabia ya kile kilichoahidiwa ilitambulikana katika Yeye.

⁹⁴ Huyu mtu hangeweza kuandika jina lake, Biblia ilisema yeye alikuwa mtu asiye na elimu, asiye na maarifa. Lakini ilikuwa utambulisho mkuu sana, hata akaungama upesi kutoamini kwake kwote, naye akasema, “Huyu ndiye Masihi ambaye tumekuwa tukimtarajia!” Vema, yeye aliamini.

⁹⁵ Kuliwako mmoja aliyekuwa amesimama hapo jina lake Filipo, aliyekimbia mjini, mlimani, na nchini, kwa umbali upatao maili kumi na tano, na akampata rafikiye, akarudi siku iliyofuata pamoja naye, jina lake Nathanieli. Alimpata chini ya mti, akiomba. Akasema, “Njoo, umwone yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

⁹⁶ Yeye alisema, “Naam, naam, naam! Laweza neno jema kutoka Nazareti, huko kwa watu duni kule chini?”

Yeye alisema, “Njoo uone!”

⁹⁷ Hilo ndilo nzuri, hayo ndiyo matamshi mazuri mno mtu angetoa. Usikae nyumbani na kulaumu. Njoo upeleleze, chunguza Maandiko! Njoo, uone!

⁹⁸ Njiani kote, wakatembea, wakizungumza kuhusu yale yaliyokuwa yakitendeka, jinsi alivyomwambia yeye kuhusu vile Simoni alivyotambuliwa Naye, babaye na kadhalika.

⁹⁹ Kisha alipokuja msitarini, labda ulikuwa mstari wa maombi, labda ilikuwa huko nje katika wasikilizaji, sijui. Lakini po pote alipotoka, Yesu alipomwona tu mara ya kwanza, akamwambia, “Tazama Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake.”

Yeye akasema “Rabi, umepataje kunitambua?”

¹⁰⁰ Yeye alisema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Hilo lilikuwa thibitisho la tabia ya Mungu mpakwa mafuta.

¹⁰¹ Akasema, “Rabi, Wewe u Mwana wa Mungu!” Ilikuwa nini? Tabia Zake zilimtambulisha. Yeye alijua kwa Maandiko kuwa huyo alikuwa yule Mtu aliyepakwa mafuta, Mungu

mpakwa mafuta katika mwili. Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake. Yeye alisema, “Rabi, Wewe U Mwana Wa Mungu. Ndiwe Mfalme wa Israeli.”

¹⁰² Yesu alisema, “Kwa sababu nilisema hayo, waniamini? Utaona mambo makuu kuliko haya.”

¹⁰³ Sasa, kulikuwepo wale waliosimama hapo, ambao hawakuamini Hayo. Wao walisema, “Mtu huyu ni Beelzebuli, Yeye yu mpiga ramli.”

¹⁰⁴ Yesu alisema, “Nawasamehe hayo. Lakini Roho Mtakatifu ajapo kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa katika ulimwengu huu au ulimwengu ujao.”

¹⁰⁵ Mnaona, upatanisho ulikuwa bado haujafanywa. Mwaona, hapangekuwako, hauwezi kuwa na...Hauwezi kutupwa kuzimuni kabla hujaletwa hukumuni. Hili taifa haliwezi kufanya hivyo, hata Mungu pia. Waona, uko mahali fulani, ukingoja katika minyororo ya kifungoni hata utakapohukumiwa. Na, mwaona, Yeye hangewafukuza, kwa sababu upatanisho ulikuwa bado haujafanywa.

¹⁰⁶ Lakini baada ya kifo Chake, kuzikwa, na ile Ishara ikatoka kwa ile Damu, yule Roho Mtakatifu, basi, kunena dhidi ya Huyo, ni dhambi isiyosamehewa. Ni neno moja tu upaswalo kunena kumpinga, ndiposa hapana msamaha po pote. Neno moja tu kumpinga, waona, ni jambo kuu vipi.

¹⁰⁷ Sasa, basi twaona tena, hili lilimtambulisha Yeye kama Masihi mpakwa mafuta. Mungu katika Kristo, aliye upatanisho wa siku hizi za mwisho. Kristo akifanya upatanisho kwa ajili ya siku za mwisho. Sasa, kwa Nathanieli, yeye—yeye, aliamini na kumtambua Yeye.

¹⁰⁸ Kulikuwa maskini mwanamke mmoja aliyekuja kisimani wakati moja huko Sikari, mji wa—wa Samaria. Yesu alikuwa na haja kupitia pale alipokuwa njiani Mwake, akishuka mlimani toka Yerusalemu kuingia Yeriko, lakini Yeye alizunguka kupitia Samaria. Alisema alikuwa “Na haja kwenda,” Baba alimwongoza hadi huko. Aendapo huko, Yeye aliwatuma wanafunzi waende. Na akaketi chini, akiwaza, nadhani, ndivyo ilivyokuwa.

¹⁰⁹ Sasa, kumbuka, Yohana 5:19, Yesu alisema, “Amini nawaambieni, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda.” Sasa kumbuka, Yeye, hakufanya muujiza hata mmoja, si wakati yeye *aliposikia*, ni “alipoona.” “Mwana hatendi cho chote hadi amwone Baba akikitenda kwanza.”

¹¹⁰ Mnaona hilo laonyesha alichokuwa, yule Nabii, Mungu-Nabii. Zaidi ya Nabii, Yeye alikuwa Mungu! Yote ambayo manabii walikuwa, yalikuwa ndani Yake, na zaidi. Manabii walikuwa tu na sehemu ya Neno. Yeye alikuwa na Neno lote, Yeye

alikuwa Neno katika utimilifu Wake, Lakini tazama, “Mungu ambaye kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi alinena katika visehemu. Katika siku hizi za mwisho, utimilifu wa Neno umekuja katika Mwanawe Kristo Yesu, Mungu aliyefanyika mwili kati yetu.”

¹¹¹ Maskini mwanamke huyu, mwenye sifa mbaya, twamwita wakati mwingine kahaba. Labda mtoto alikuwa ametupwa nje barabarani. Labda kama ilivyo sasa, si hatia za vijana pekee, ni hatia za wazazi, kumwacha maskini bibi fulani aondoke na kutenda hivyo. Labda maskini msichana mrembo, alienda pale kuchota ndoo moja ya maji, yapata saa tano.

¹¹² Sasa kumbuka, ikiwa umewahi kuwa mashariki, hawajabadilika hata kidogo, zingali ni desturi zile zile. Wanawake huenda, bikira huenda asubuhi visimani na kuteka maji yao, kahaba au mwenye sifa mbaya havezi kwenda pamoja nao. Hawawezi kuchangamana.

¹¹³ Ilimlazimu aje baada ya wengine kumaliza. Yeye alikuja, labda amechoka, labda alikuwa na huyo kijana rafiki mpya, mume wake usiku huo. Naye akaja, alikuwa na chungu hiki, akakiweka chini. Akakiweka, kwenye mtambo wa kuinulia, akakitelemla, yeye akasikia Mwanamume yule akisema, “Nipe maji ninywe.”

¹¹⁴ Huyo mwanamke alitazama na kuona Mwanamume wa makamu amesimama hapo, mwenye mvi. Yeye alikuwa tu mwenye umri upatao miaka thelathini, lakini Biblia yasema alionekana kama wa miaka hamsini. “Wewe ni mtu asiyeipita umri wa miaka hamsini. nawe wasema umemwona Ibrahimu?”

¹¹⁵ Yeye alisema, “Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO” Mwaona? Mnaona, hawakuelewa Hilo. Yeye alikuwa akiwatikisa hao wanyonyaji watoke Kwake.

¹¹⁶ Siku hizi yatubidi kusihi na kuwaomba, na kuwabembeleza na kuwasihi, na kuwashawishi na kuwaahidi Wakristo, waje kanisani, “Wakija kanisani, tutafanya hiki na kile.”

¹¹⁷ Yesu, alipokuwa duniani, alikuwa na wengi mno pamoja naye. Yeye alitazama hapa na pale na kuona umati, alitaka kuwafukuza, Naye akasema, “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu.”

¹¹⁸ Ungeweza kuwaza daktari akiketi pale? “Naam,” akasema, “Mtu huyu atutaka tuwe wafyonza damu. Eti tunywe Damu Yake? Upuzi! Ninyi nyote ondokeni na mmwache Mtu huyo mwenye wazimu pekee.” Wakaondoka.

¹¹⁹ Yeye hakuyaeleza. Haikumbidi aeleze. Yeye mara nyingine hutikiza imani yako aone utakachofanya. Naye anatenda jambo lile lile leo, naam, na kuifanya ionekane kidogo kama kwamba ni ya kimizimu kwako, kuona msimamo wako ulipo, ikiwa waamini hakika.

120 Kumbuka, hao wanafunzi, waliochaguliwa awali na Mungu, hawakuondoka kamwe. Wao hawangeweza kulieleza, pia, lakini hawakutaka kuondoka. Ndipo Yeye aja tena, akasema . . .

Makutano hao wote waliondoka, maelfu.

121 Akawaambia sabini walioketi hapo, watumishi Wake aliowachagua waende na kuhubiri mbele Zake. Yeye alisema, “Nitawatikiza nione mahali walipo.” Basi Yeye akasema, “Vema, mtasemaje basi, mmwonapo Mwana wa Adamu akipaa juu Mbinguni alikotoka?”

122 “Mwana wa Adamu akipaa mbinguni? Tunavua samaki pamoja Naye, tunalala kwenye kingo za mto pamoja Naye. Tunakula pamoja Naye. Tumeona hori alimozaliwa. Twajua mama Yake, Ndugu Zake. Na huyu Mwana wa Adamu akipaa juu alikotoka? Yeye alitoka Nazareti! Haya ni maneno magumu.” Waliondoka pia. Wao walisema, “Hatuwezi kufahamu Haya.” Mwaona? Kipi kilitendeka? (Halikuwatikisa wanafunzi. Hawangeweza kulieleza.) Wote waliondoka. Yeye hakulieleza. Haikumbidi alieleze.

123 Siku hizi tuna mimea ya tuta, iitwayo Wakristo, mtu fulani ambaye yakubidi kumnyunyuzia maji na kumlea na kumfurahisha, “Na utanipa ushirika, utashirikiana, utafanya *hili*.” Loo, enyi mimea ya tuta! Twahitaji Ukristo halisi, uliozaliwa na Roho wa Mungu. Nao huo hautachukua ushirikiano, wala cho chote kile, hawataki cho chote.

124 Yesu aligeuka, akawatazama hao wanafunzi, akasema, “Nanyi mtaondoka pia? Mwataka kwenda zenu pia?” Yeye alisema, “Nimewachagua ninyi kumi na wawili, na mmoja wenu ni ibilisi. Mbona msiondoke pia?”

125 Ndipo Petro akasema hayo maneno ya kukumbukwa, “Bwana! Tungeenda wapi? Tumeshawishika, twajua kuwa Wewe u chemchemi ya Uzima iliyothibitishwa. Unalo Neno, na hilo pekee. Tumeshawishika.”

Maskini mwanamke huyu akisimama pale. Kasema, “Niletee maji ninywe.”

126 Yeye akasema, “Sio desturi, tuna ubaguzi, hatuna kitu kama hicho hapa.”

127 Yeye alimfanya aelewe upesi kuwa hakuna tofauti kati ya Myahudi au ye yote yule. Yeye alikuwa Mungu. Naye alisema, “Nenda ukamlete mume wako na mje hapa.”

Alisema, “Sina mume.”

128 Yesu alisema, “Umesema ukweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye si wako.”

129 Sasa tazama mwanamke huyo. Kitu fulani kilitendeka, hiyo Mbegu ndogo iliyochaguliwa awali humo moyoni mwake!

¹³⁰ Alipoyasema Hayo kwa hao Mafarisayo, watazame, walitiliwa giza yale waliyokiri. Walikiri kuwa Wakristo, walikiri kuwa wafuasi, walikiri kuwa wanampenda. Lakini Ukweli ulipokuja, uliwatia giza.

¹³¹ Lakini hili lilipokuja, likaihuisha, likaondoa weusi na kufanya yote nyeupe. Kasema, “Wapi . . .”

¹³² Yeye akasema, “Bwana, naona kuwa U nabii. Sasa hatujakuwa na nabii hata mmoja kwa muda wa miaka mia nne, waona. Naona kuwa U Nabii. Sasa, twajua kuwa Masihi ajapo, kitambulisho Chake kitakuwa tabia ya aina hiyo. Naye atatwambia mambo haya.”

Yeye alisema, “Ndiye Mimi ninayenena nawe.”

¹³³ Na, kusikia hayo, akatupa mtungi wa maji, akaenda mjini na kusema, “Njooi, mmwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Je, si hizi ni tabia zile zile za Masihi mpakwa mafuta ambaye ni Neno, lijualo mawazo yaliyomo moyoni? Je, si huyu ni Masihi?” Lo, jamani!

¹³⁴ Tazama, mwanamke aliyekuwa akitokwa damu, Yeye alitambulikana kwake, kwa tabia Zake, kuwa Yeye alikuwa Masihi. Mwanamke ambaye alikuwa akitokwa na damu alimtambua Yeye, aliye Neno.

¹³⁵ Waebrania 4:12, Biblia ilisema kuwa, “Neno la Mungu lina nguvu kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, na hutambua mawazo yaliyomo moyoni,” (Wangapi wajua hayo?) “Katika mawazo.” Hivyo ndivyo Neno lilivyo. Mwaamini Yeye alikuwa lile Neno? Je, mwaamini Yeye ni Yeye yule jana, leo na hata milele? Hilo latosha, ikiwa mwaamini Hilo.

¹³⁶ Tazama, maskini mwanamke huyu alisema, “Nikiweza tu kungusa! Sijali wasemaje juu Yake. Naamini kuwa Yeye yu tu kile alichosema alikuwa. Nikimgusa, nitapona.” Kwa hivyo yeye akapenyeza na kungusa. Akarudi tena kwenye umati.

Yesu akasimama, na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

¹³⁷ Na Petro alijaribu kumfanya Yeye kama mtu mwenye wasiwasi, akasema, “Kwani, kila mtu! Usiseme mambo kama hayo, naam, hawatajua watakachokuwazi Ni Mtu wa daraja Yako, kisha useme, ‘Ni nani aliyenigusa?’ Kila mtu anakugusa.”

¹³⁸ Yeye akasema “Lakini naona ya kuwa nimekuwa mdhaifu, nimetokwa na nguvu.” Alijua kitu fulani kilikuwa kimetendeka!

¹³⁹ Sasa tazama, tazama kile kinachokuja, mshituko mkuu unaofuatia. Yeye alitazama hapa na pale hadi akamwona, naye akamwambia hali yake, na kuwa imani yake ilikuwa imemwoko. Huyu mwanamke alikuwa . . . Yesu alitambulikana kuwa lile Neno la Mungu, akijua siri za moyo. Lo, jamani! Neno hutambua mwili, hutambua moyo.

¹⁴⁰ Sasa kwa muda mfupi tu, katika kufunga. Sasa, kama Waebrania 13:8 ilivyo kweli, “Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele,” je unaamini Hilo? Sasa ninayaacha mengi hapa ambayo ningesema. Basi tabia Zake zitamtambulisha Yeye sasa katika wakati uu huu, ikiwa ni Yeye yule jana, leo na hata milele, kama tu vile alivyokuwa wakati huo. Je, hilo ni sahihi? Yeye ameliahidi. Na, kumbuka, Tabia Zake ni kitambulisho Chake. Wangapi wanalielewa, inueni mikono yenu. Tabia Zake ni kitambulisho Chake.

¹⁴¹ Kama wale waliotoka Emau, ninaposema hili. Yesu amekwisha kusulubishwa. Wao wote walikuwa na huzuni. Walikuwa huko kaburini, basi walisema, “Mtu fulani alikuja na akamwiba.” Siku moja Yeye alitoka vichakani na kutembea pamoja nao, alipokuwa akienda Emau. Nao wakasema . . .

Yeye alisema, “Mbona ninyi mmehuzunika sana?”

Akasema, “Vema, wewe u mgeni hapa?”

¹⁴² Naye alipowaleta ndani, alifanya kitu fulani kama tu alivyofanya kabla ya kusulubishwa Kwake. Ilikuwa ni tabia Yake kufanya hivyo. Nao mara wakamtambua, kwa tabia Zake, kuwa huyo alikuwa ni Yesu yule yule aliyekuwa amesulubishwa. Amina.

¹⁴³ Mungu amemfufua toka kwa wafu, na leo tabia Zake, ziko tu, kama vile zilivyokuwa wakati huo! Na kurudi kwa siku za Sodoma, kama Yesu alivyotabiri, jambo lile lile litatendeka “wakati Mwana anapofunuliwa kwa watu.” Ni thibitisho la tabia Zake. Waebrania 4:14 na 15, “Yeye sasa ni Kuhani wetu Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu, kama tu alivyokuwa wakati huo.” Je, mwaamini hilo? Udhaifu wetu hungusa. Vema, kama ungemgusa Yeye, angefanyaje ikiwa Yeye ni Yeye yule jana, leo na hata milele? Tabia Zake zingekuwa zile zile. Ndipo Yeye angetenda kama alivyotenda wakati mwanamke yule alipogusa vazi lake. Je, mwaamini hilo? Yeye aishi daima, Yeye ni yule aishiye, na tabia Zake zingali zamthibitisha Yeye kama tu vile alivyokuwa wakati huo. Je, mwaliamini kwa mioyo yenu yote? Mungu, akitambulishwa na tabia Zake, zinamtambulisha.

Tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁴⁴ Baba aliye Mbinguni, sisi ni wanaume na wanawake tu tunaoketi hapa usiku huu. Lakini sisi, kama ilivyokuwa, tunampapasa-papasa Mungu tunapolitumia Neno. Na, Baba, ningegopa kujaribu kusema kitu ambacho hakikuwa ndani humu. Ningegopa kujaribu kuweka tafsiri yangu mwenyewe kwa hilo Neno, kwa sababu ingekuwa makosa. Nawe ulisema, “Ye yote atakayeondoa Neno moja Kwake, au aongeze neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa toka kwa kile Kitabu cha Uzima.” Maisha yangu yatakuwa na manufaa gani wakati

huo, Bwana, nikitenda kitu kiovu kama hicho? Kwa hivyo mimi nalinena tu jinsi lilivyo.

¹⁴⁵ Na, Baba, uliahidi kuwa ungelithibitisha. Naamini kuwa umefufuka toka kwa wafu, miaka elfu mbili iliyopita, nawe u hai usiku huu, ukiwaita watu wa kawaida kama vile umefanya daima, mmoja hapa na mmoja pale; si makundi, si madhehebu, si mambo makuu ambayo mwanadamu alitenda. Lakini Wewe ulisema utawatoa watu kati ya mataifa, watu fulani, “Wawili shambani; nitamwacha mmoja, na kumchukua mmoja. Wawili kitandani; nitamwacha mmoja, na kumchukua mmoja,” watu hapa na pale, kwa ajili ya jina Lako, yule Bibi-arusi.

¹⁴⁶ Naamini kuwa tabia Zako zinakutambulisha Wewe. Wewe uliahidi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” ndivyo itakavyokuwa katika siku utakapofunuliwa, lile Neno. Neno Lenyewe, la wakati huu, lapaswa lifunue Neno Lenyewe, kama vile Neno lilivyowajia manabii. Na, Baba, twamuona Yohana akisimama hapa duniani, na palikuwepo na lile—lile Neno ambalo alikuwa akilifunua. Na Biblia ilisema, “Neno kila mara humjia nabii.” Nalo Neno lilikuwa mwili wakati huo, kwa hivyo lilitembea moja kwa moja hadi majini, kwa Yohana. Neno lilimjia nabii.

¹⁴⁷ Baba Mungu, njoo usiku huu naomba, ukatusaidie. Saidia kutokuamini kwetu. Utusamehe makosa yetu. Ponya wagonjwa na wanaoteseka. Neno moja toka Kwako, Bwana, litamaanisha zaidi kuliko cho chote mtu ye yote angesema. Nena tu, Baba, Neno moja tu litafaidi sana. Sasa, Wewe U Yeye yule jana leo, na hata milele. Twajikabidhi Kwako sasa. Nasi twaomba kuwa tuondokapo na kuenda manyumbani mwetu usiku huu, tutasema kama wale waliotoka Emau, walipomwona akitenda kitu fulani aonyeshe kwao kuwa Yeye alikuwa Bwana aliyefufuka. Haijalishi walisema mara ngapi, “Wao waliuiba mwili Wake, na—na walifanya *hili, hilo*, au *linginelo*,” wao wenyewe walijua kuwa Yeye alifufuka toka kwa wafu. Mbona usiku huu usijionyeshe Mwenyewe kwetu hai tena, na uwaite wale walio katika mji huu mzuri na vitongoji vyake, wale walioteuliwa kwa Uzima, waje Kwako. Kwa kuwa twaomba katika jina la Yesu. Amina.

¹⁴⁸ Sasa, nitawauliza sasa kwa dakika zipatazo kumi na tano hivi. Tutachelewa kwa dakika kama kumi hivi. Nitaharakisha. Nataka kuita kadi za maombi. Naamini Billy...G, kadi za maombi G, je, hizo ndizo zilizotolewa? G, kadi za maombi G, hebu tuchukue moja hadi kumi na tano ama ishirini, ama zaidi. G, moja. Ni wangapi...Nani ana G, nambari moja, inua mkono wako, angalia kama iko hapa. [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] Na, kumbukeni, shikilieni kadi zenu za maombi, mtaombewa. Usipoipata usiku huu, tutaipata. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, njooni hapa upesi mwezavyo, na mje moja kwa moja hapa mwingie mstarini. Vema.

Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Watatu hawapo hapa. Saba, saba, na moja, mbili, tatu, . . . Wahesabu, Roy, kwa niaba yangu. Vema, kumi. Vema, moja hadi kumi. Kumi na tano sasa, G, moja hadi kumi na tano, hiyo ni kumi na ta . . . au kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Vema. Hebu—hebu tukome hapa, hawa tu. Vema.

¹⁴⁹ Sasa tuna—tunajaribu kutunza neno letu, mwaona, tuondoke ifikapo saa tatu na nusu, lakini hatutafanya hivyo usiku huu, na—na—najua. Lakini nataka kila mmoja anisikize kwa makini sana.

¹⁵⁰ Sasa ikiwa nimesema Ukweli na kuwaambia kuwa mambo haya yapaswa kuwa, na ndiyo haya katika Biblia, kuwa huu ndio wakati. Yawezekana umefunzwa katika shule nyingine. Hata na Mafarisayo pia. Lakini Biblia ilisema, katika siku hiyo, “Bikira atachukua mimba,” Yeye . . . Naye akachukua. Yeye alisema tabia za Masihi zingekuwa hivyo. Zikawa. Lakini wao hawakuamini. Hilo halikumzuia kuendelea vivyo hivyo tu. Kama ilivyo sasa. Tunaishi katika majira ya mwishoni ya siku ya mwisho.

¹⁵¹ Sayansi husema ni usiku wa manane kasoro dakika tatu. Nadhani imekaribia zaidi ya hivyo sasa, wakati wo wote. Ukomunisti umejipenyeza nchini, nao wahubiri wameuendea Ukomunisti badala ya Kristo. Yaonekana kama kuondoka kwenda kujaribu kuudhulumu, mbona hawaoni saa tunayoishi? Ukomunisti, hatuna . . . Loo, salala! Mimi siogopi Ukomunisti. Ni kuja kwa Bwana kutakakowakuta hamjawa tayari, hilo ndilo jambo, kwa kanisa. Sasa hebu kila mtu, hebu Amerika yote na imrudie Mungu, na utazame kile kingetendeka kwa Ukomunisti. Lazima utambue maradhi ndiposa upate uponyaji.

¹⁵² Sasa, kila mtu awe mnyenyekevu, tafadhalini msitangetange. Sasa, wangapi huko hawana kadi za maombi, nanyi mwataka Mungu awaponye, hebu inueni tu mikono yenu, sema, “Ni—ni—ni—ninaamini.” Haijalishi uko wapi.

¹⁵³ Sasa tazameni, nadhani hii inafanya kazi [Ndugu Branham apuliza katika maikrofoni—Mh.] hii. Vema. Ikiwa mwaweza kunisikia huko nyuma? Vema. Vema. Sasa tazama, Ndugu Roy.

¹⁵⁴ Sasa Neno moja toka kwa Mungu lafaa zaidi kuliko yote ningeliweza kusema.

¹⁵⁵ Sasa, kutazama toka hapa, ni vigumu, hii—hii kila mara ilikuwa hivyo. Mwaona, taa zinanitia kiwi, na ni vigumu kutazama kule kuwaona watu.

¹⁵⁶ Nami sijui. Siwezi kumwona mtu hata mmoja, hakika, ninayemwona sasa nimjuaye. Ni wangapi walio wageni kwangu, inueni mikono yenu, wajuao sijui cho chote kuwahusu. Nadhani ni kila mahali. Wangapi katika mstari wa maombi wanaojua sijui cho chote kuwahusu, inueni mikono yenu. Wote kwenye mstari wa maombi hapo, ikiwa mwaweza kunisikia, inueni mikono yenu ikiwa—ikiwa mimi ni mgeni. Kila mmoja.

¹⁵⁷ Sasa Yeye ni Nani? Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. Huyu mwanamke aliyegusa vazi Lake, labda yeye hakuwa na kadi ya maombi, pia, lakini alimgusa Yeye na, alipomgusa, kitu fulani kilitendeka. Sasa wewe gusa kwa njia ile ile, mguse. Wangapi wajua Waebrania, sura ya 4, inasema, “Sasa Yeye yu Kuhani Mkuu awezaye kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu?” Wangapi wanajau vile? Vema, Yeye angeonyesha waziwazi tabia Zake zile zile? Ikiwa ni yeye yule jana, leo na hata milele, Yeye atafanya hivyo. Vema, sasa, hii ni ile. . .

¹⁵⁸ Ndugu Peary, waletе kwangu sasa. Sasa nataka kila mtu awe mnyenyekevu sana. Papa hapa, papa hapa tu, dada.

Sasa, mwaweza kunisikia? Sasa, sijui, wewe tazama ye yote aliye kwenye—fundi wa mitambo pale, kwa sababu sijui vipi.

¹⁵⁹ Ono. Sasa kumbuka, mimi siye Masihi, mimi siye Kristo. Lakini Yeye yuko hapa. Hilo ndilo ninalojaribu kuwafanya muone, Yeye yuko hapa, Yeye hulinda Neno Lake.

¹⁶⁰ Sasa, ikiwa mwanamke huyu yu mgonjwa, sijui. Simjui. Yeye ni mzee kuliko mimi. Pengine tumeachana kwa miaka mingi, na maili nyingi, huu ndio wakati wetu wa kwanza kukutana.

¹⁶¹ Sasa, hivyo ni kama tu Bwana wetu alipomkuta fulani, mwanamke, katika Injili ya Yohana 4. Najaribu kuifanya dhahiri sana usikose kuiona, ndipo, Mle Hukumuni, hapatakuwa na damu mkononi mwangu siku hiyo. Sasa, Yesu aliahidi kuwa katika siku za mwisho hili lingetukia tena. Tunapoendelea katika juma hili, utatambua kuwa ni ahadi.

¹⁶² Sasa, simjui huyu bibi, huyu ni mwanamume na mwanamke wanaokutana kwa mara ya kwanza. Sasa, ikiwa Bwana Yesu atanifunulia kile kilichokuleta hapa, au mtu ye yote yule, au kile unachotenda, au shida yako, au kile umetenda, ikiwa ni fedha, mambo ya nyumbani, cho chote kile, lazima itoke kwa Nguvu za kimbinguni, kwa sababu sikujui. Wangapi watashuhudia hilo, kuwa lazima lipitie kwa Nguvu za kimbinguni? Sasa, mwaweza kuyapuuza kama Mafarisayo, kusema ni . . . (Zungukia upande mwingine, Ndugu Roy, waona.) Mwaweza kuyapuuza kama Mafarisayo, na kusema, “Ni pepo mchafu,” ambayo wengi hutenda. Hilo ni kati yako na Mungu, basi. Ndiposa una thawabu yao. Lakini ukisema, “Ni la Mungu,” basi una thawabu Yake. (Sasa, hilo ni bora, mnaona.)

¹⁶³ Sasa nitazame tu kwa dakika moja hivi. Kama Yesu alivyosema. . . Kama Petro na Yohana walipopitia kwenye mlango wa hekalu uitwao Mzuri, kasema, “Nitazame.” Si—sikujui. Na sasa ikiwa Roho Mtakatifu, Mtu fulani zaidi yangu, atakuja afunue kile kilicho moyoni mwako, basi Biblia yasema, “Neno la Mungu li kali kulilo upanga ukatao kuwili, hutambua mawazo, makusudi ya moyo.” Hivyo ndivyo hasa Biblia isemavyo. Sasa, hilo hufunua basi siri za moyo. Sasa, hiyo

ingekuwa tabia ya Mungu, Neno lililodhihirishwa katika siku hizi. Wangapi wanaamini hilo sasa? Sasa unaona lilivyo?

¹⁶⁴ Sasa nimelihubiri, nimewaambia kulihusu, lakini je, hilo ni kweli? Hilo ndilo jambo linalofuata, waona. Sasa, ikiwa ni kweli, kila mmoja wenu. . . Ikiwa si kweli, huyu mwanamke atajua. Hakika, atajua. Mtajua pia. Lakini ikiwa si kweli, basi nime—ni—nimemshuhudia Kristo uongo. Ikiwa ni kweli, kila mmoja wenu yambidi ampe Yeye moyo wake, yakubidi umwamini kwa moyo wako wote, na umwendee na kumkubali Yeye kwa cho chote unachohitaji. Hilo ni kweli.

¹⁶⁵ Na Roho Mtakatifu sasa ajitambulisha Mwenyewe katika jina la Yesu Kristo. Sasa, sina habari ni nini kilichokuleta hapo. Waonekana tu kama mwanamke mrembo, aliye kama mama anayesimama pale, na hayo tu ndiyo ninayojua kukuhusu wewe. Lakini Roho Mtakatifu aweza kuonyesha kilichokuleta hapa, shida yako ni nini, cho chote kile. Utajua kama ni kweli au la. Sasa, wewe, unachotakia maombi, ni kitu kama misuli ya uso wako. Ni maradhi ya neva usoni mwako. Sasa, ikiwa hayo ni kweli inua mkono wako. Je, unaamini?

Naam, sasa waweza kusema, “Yeye alibahatisha tu hilo.”

¹⁶⁶ Naam, yeye ni mtu mwenye afya pia. Sasa, Bibi, tazama hapa kwa muda mchache, dada. Sijui kile Yeye alikwambia. Lakini cho chote alichokwambia, kilikuwa kweli. Wewe u shahidi wa hilo sasa, siyyo? [Yule dada asema, “Hilo ni kweli.”—Mh.] Hilo ni kweli. [“Kwa miaka ishirini.”] Lo! Unaamini kuwa Mungu atakuponya huo? Sasa, wajua ni Uwepo Wake, kuna Kitu fulani hapa kikujuacho wewe, Kitu fulani. Kama Yesu alivyomwambia yule mwanamke, Yeye alijua ambapo shida yake ilikuwa, naam, Yeye ajua shida yako ilipo.

¹⁶⁷ Na yaonekana umelemewa kwa ajili ya mwingine. Ni. . . Ni mwanamume, ni mumeo. Yeye yuko hapa pia. Hayo ni kweli. Na—na unaamini kuwa Mungu aweza kufunua shida ya mumeo kwangu? [Yule dada asema, “Ndivyo, naamini.”—Mh.] Yeye yu mgonjwa sana, ugojwa wake unatatiza. Kitu kimoja kinachomsumbua, ni shida ya moyo. Yeye ana ugonjwa wa moyo. Ikiwa hilo ni kweli, inua mkono wako. [“Hilo ni kweli.”] Yeye pia ana maradhi ya mshipa. [“Hayo ni kweli.”] Hayo ni kweli. Si hayo ni kweli? [“Naam, hayo ni kweli.”] Yeye huwa na wasiwasi sana, naam, ana wasiwasi. Hayo ni kweli, au siyyo? [“Naam.”]

¹⁶⁸ Ikiwa Yesu atanifunulia! Yeye alimwambia Petro alikuwa nani. Ikiwa Yeye atanifunulia wewe u nani, je, utaamini kuwa ni Yeye? [Yule dada asema “Ndiyo.”—Mh.] Wewe hautoki hapa. [“La.”] Watoka mashariki ya hapa, unatoka Louisiana. [“Sawa.”] Hilo ni sawa. Vema. Na jina lako ni Bi. Coleman. [“Hilo ni kweli.”] Rudi nyumbani, Yesu Kristo akuponya. Imani yako yakuponya.

169 Sasa aminini. Je, mwaamini kwa mioyo yenu yote? Yesu Kristo akijitambulisha Mwenyewe katika kufufuka Kwake! Mwakiona ninachomaanisha? Sasa, ye yote mwenye akili za kawaida, ajua kuwa hakuna mwanadamu awezaye kufanya hilo.

170 Sasa, ninyi huko nje, mwambieni Mungu hivi, “Ni—ni—ninajua mtu huyu hanijui, kwa hivyo nitaombea kitu fulani. Bwana, je, naweza kugusa vazi Lako? Ikiwa ni hivyo, basi jitambulishe katika kufufuka Kwako. Geuka, hebu nikuguse, na ndipo unene nami kupitia kwake.” Uone kile kitakachotendeka. Hebu jaribu tu.

171 U hali gani, bwana? Waweza kukaribia hapa kidogo? Kuna watu huko nyuma yako huko, waona.

172 Kila kitu sasa, ni kila—kila roho ni kama mpumo. Waishika, mwaona, pia wajua mawazo yao, nayo huwa, waona, unatatanishwa.

173 Je, unaamini mimi ni mtumishi Wake? Je, waamini kuwa Kristo aweza kunifunulia kile kilichokuleta hapa? Kumbuka, tutakutana Hukumuni siku moja na kutoa hesabu ya usiku huu. Wafahamu hilo? Shida yako, moja yazo, iko mgongoni mwako. Una shida nyingi. Una maumivu ya mgongo. Na macho yako yanafifia, una shida za macho. Ikiwa hayo ni kweli, inua mkono wako. Naam, wewe pia unatenda jambo fulani ambalo ungetaka uepukane nalo. Je, ni vema kwangu kulitaja? Wataka uache kuvuta sigara. Na—na kitu kingine, umekuwa na . . . wajisikia kuwa hicho ndicho kitu ambacho kimekuzuia usimpokee Roho Mtakatifu. Sasa wataka kumpokea Roho Mtakatifu, hiyo ndiyo hamu moyoni mwako. Hilo ni kweli, pungu mikono yako hivi. Vema, imekuondokea sasa, nenda ukampokee Roho Mtakatifu, na uponywe katika Jina la Yesu Kristo.

174 Mwaamini? Sasa tafadhali iweni wanyenyekevu kabisa. Sasa tunachelewa sana, tulieni tu kwa muda mfupi.

175 U hali gani? Sisi tu wageni mmoja kwa mwingine. [Yule dada asema, “Ndivyo.”—Mh.] Bwana Yesu atujua sote wawili. Sasa usiwe na uoga, waona, yaonekana unao. Waona, tulia tu, ni Uwepo Wake. Unaona, liko hivyo hakika. Ni Uwepo Wake. Sasa unajisikia ajabu, ah, ni kuzuri, kujisikia kwa aina ya unyenyekevu. Waona? Sasa, kusimama mbele ya mwanadamu hakungekufanya ujisikie hivyo.

176 Wangapi wamewahi kuona hiyo Nuru, hiyo Nguzo ya Nuru, Moto? Ilichukuliwa papa hapa Texas, mara ya kwanza, mara ya pili. Sasa inaning’inia juu ya huyu mwanamke, mwaona, kwa kiwango hiki sasa. Laiti, laiti, mngeliiona tu.

177 Uanzapo kwenda, hiyo ndiyo inayoisababisha, unaona. Kesho usiku tutakuwa na huu mstari wa maombi kabla ya saa tatu, mnaona, ni—ninawakawisha sana. Hebu tumwombe huyu mwanamke mmoja, basi. Hebu kidogo.

178 Waamini, unayeketi hapo? Naam, kwa huo udhaifu unaokusumbua, hiyo ndiyo shida. Mnaona? Yeye aligusa nini? Simjui huyu mwanamke. Yeye alimgusa Kuhani Mkuu. Lakini, mnaona, nilikuwa nimemwelekezea mgongo wangu, kama tu vile alivyofanya wakati wa Ibrahimu. Hapa, tazama hapa, dada, kwa muda mfupi. Waonekana unalemewa moyoni mwako. Ndiyo. Ni binti yako nyuma huko. Yeye ana shida katika masikio yake. Hilo ni kweli. Waamini sasa kwa moyo wako wote? Vema, amini tu sasa, naye atapona.

179 Mnaona ninalomaanisha? Ukiamini, vitu vyote vyawezekana. Je, waamini?

180 Kuna maskini bibi ambaye amerudisha chini mkono wake nyuma hapo, yeye ananitazama. Yeye anaugua ugonjwa wa sukari. Je, waamini kuwa Mungu atauponya ugonjwa huo wa sukari, ukiketi hapo? Vema, waweza kupata kile unachoomba, basi, amini tu.

181 Bibi aliye nyuma yako, ana ugonjwa wa chango na maumivu ya kibofu. Je, waamini kuwa Mungu ataponya hayo, atakupa afya? Vema, waweza kupata kile unachoomba. Mkono wa maskini bibi huyu. Mwaona, tazameni sasa, muulizeni yeye, kitu fulani kizuri kimemgusa. Mwaona, imani yake, hiyo ndiyo inayofanya hivyo. Si mimi. Ni Mungu.

182 Naam, hapa kuna mwanamume ambaye ameketi papa hapa mwishoni. Yeye ana maumivu ya kifua, huyu mzee anayeketi hapa akinitazama. Je, waamini kuwa Mungu atakuponya, bwana? Huyo mwanamke karibu nawe anaugua ambukizo mwilini mwake. Hayo ni kweli, dada, peperusha kitambaa chako ikiwa hilo ni kweli. Vema, vema, ninyi nyote wekeaneni mikono yenu mmoja kwa mwingine, aminini kwa mioyo yenu yote. Baba, binti, mbona isiwe hivi? Wekeaneni mikono yenu mmoja kwa mwingine na aminini kwa mioyo yenu yote, Yesu awaponya.

Ni—nawahimiza imani yenu mliamini!

183 Mwanamke anayeketi hapo nyuma yake, ana ugonjwa wa tumbo. Je, waamini kuwa Mungu atakuponya, bibi? Hiyo ndiyo shida yako. Ikiwa hilo ni kweli, simama ili watu waone. Mnaona? (Wao wanamgusa nani huko?) Aisee, sijakosea, hapo yuko mama yako anayeketi kando yako hapo. Naye ana ambukizo katika matumbo yake. Waamini kuwa Mungu ataponya hayo bibi? Simama, pia, ukaponywe.

184 Aminini! Ni yeye yule jana, leo na hata milele. Yeye hujitambulisha Mwenyewe. Waniamini mimi kuwa nabii Wake, au mtumishi? Hilo huwakwaza watu, kusema “nabii,” hawalielewi.

185 Tazama hapa. Je, waamini kwa moyo wako wote? Una wasiwasi mwingi kupindukia. Je, waamini naweza kukwambia kilichousababisha? Ulikuwa na ajali ya motokaa. [Huyo dada asema, “Hilo ni kweli.”—Mh.] Hilo ni kweli. Naam, ajali ya

motokaa, mgongo wako na mabega yako. Je, hilo ni kweli? Utakuondokea sasa. Ni wakati wa maisha tu ambao pia umeusumbua, ukauchochea, lakini utapona. Enda, amini kwa moyo wako wote. Yesu Kristo atakuponya ikiwa utaamini. Ukiamini. Amina.

¹⁸⁶ Je, waamini? Waamini Yeye aweza kuponya hiyo yabisi kavu? Vema, endelea kutembea basi, Yeye atakuponya.

¹⁸⁷ Wangapi wanaami kwa mioyo yao yote, semeni, “Naamini hakika kwa moyo wangu wote”? Ukiamini tu!

¹⁸⁸ Je, waamini Yeye huponya ugonjwa wa sukari na kuwafanya watu wazima, wakiwa na ugonjwa wa sukari, na kuwaponya? Je, waamini hilo? Endelea tu, sema, “Bwana, nakushukuru kwa ajili yake.” Amini kwa moyo wako wote, nawe utaponywa.

¹⁸⁹ Ni wangapi wanaoamini huko nje sasa, kwa mioyo yenu yote? Msifanye hivyo, mwaona mnatangatanga, mnavunja utaratibu Wake, marafiki. Nitawaambia, ni wangapi wanaamini? Hebu inua mkono wako, useme, “Naamini kwa moyo wangu wote.”

¹⁹⁰ Sasa nitawauliza mfanye kitu fulani. Sasa, ikiwa Yesu amelidumisha Neno Lake, na mnaamini hilo, naye amewathibitisha, Yesu pia alisema hili, Agizo Lake la mwisho kwa kanisa Lake, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa wangapi wanaamini? Yeye alisema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Je, waamini ahadi hiyo? Basi weka mikono yako juu ya mtu fulani aliye karibu nawe.

¹⁹¹ Asipokuponya, utakufa. Umetiwa kivuli. Lakini Yesu Kristo akuponya. Je, unaamini? Vema, wekeni. . . endelea na kuamini sasa, nawe utapona.

¹⁹² Njoo bibi. Je, waamini kuwa Mungu ataponya ugojwa huo wa kifua kikuu na wa sukari, akupe afya? Twaa. . . Vema, enda, amini kwa moyo wako wote, na upone.

¹⁹³ Kuomba, je, mnaombeana? Wekeaneni mikono yenu mmoja juu ya mwingine, na tuombe, sote pamoja. Kila mtu wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine. Tumechelewa. Wekeaneni mikono mmoja juu ya mwingine na tuombe.

¹⁹⁴ Bwana Yesu, tuna hakika kuwa Mungu hujitambulisha Mwenyewe kati ya watu Wake. Tabia Zake, ni zile jana, leo, na hata milele, zinajidhihirisha zenyewe. Ee, Bwana Mungu, Wewe uliyetoa ahadi ya Neno, ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Watu hawa wamekiri kuwa waamini, waamini katika Yesu aliyefufuka Ambaye anajitambulisha Mwenyewe sasa kwa tabia Zake zile zile alizokuwa nazo alipokuwa hapa duniani, akiyafanya Maandiko yawe Ukweli halisi, kuwa ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Bwana Yesu, pamoja na waamini hawa waliowekeana mikono, katika Uwepo wa Kiungu, Mwana wa Mungu aliyefufuka na aliyethibitishwa,

ambaye amefanyika mwili tena kati yetu usiku huu katika mwili wa waamini Wake, naamuru kila pepo mchafu, kila ugonjwa na maradhi, yawaondokee watu hawa, wakati hawa waamini wanapowekeana mikono mmoja juu ya mwingine. Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo.

¹⁹⁵ Wale wote watakaoamini uponyaji wao sasa, wanaoamini hivyo wakati u huu, katika Uwepo uliothibishwa wa Mwana wa Mungu aliyefufuka, ambao wanaamini kuwa wametimiziwa haja zao, na watatambua kitu kile kile, simameni na kusema, “Nazipokea kwa moyo wangu wote.” Simameni kila mtu, katika Uwepo wa Yesu Kristo, wale watakaoamini. Msifuni! Mpeni sifa na utukufu. Inueni tu mikono yenu na mushukuru. Mungu ataimarisha kila ahadi aliyoahidi.



MUNGU HUTAMBULIWA KWA TABIA ZAKE SWA64-0311
(God Is Identified By His Characteristics)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano juoni, Machi 11, 1964, kule Beaumont, Texas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2014 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org